



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA

HALMASHAURI YA WILAYA YA NYANG`HWALE



Barua pepe: ded.nyanghwaledc.go.tz
Tovuti: www.nyanghwaledc.go.tz

Kumb. Na. AC/12/214/85

20/06/2024

TANGAZO LA NAFASI YA KAZI

Halmashauri ya Wilaya ya Nyang`hwale kupitia kibali cha ajira mbadala chenye Kumb.Na.FA.228/613/01/C/019 cha tarehe **20 Mei, 2024** kutoka kwa Katibu Mkuu Ofisi ya Rais - Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kuhusu ajira mpya. Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Nyang`hwale anatangaza nafasi ya kazi na anakaribisha maombi kwa Watanzania wenyewe sifa ya kujaza nafasi ilivyoordheshwa katika tangazo hili: -

1.0 MTENDAJI WA KIJIJI DARAJA LA III - NAFASI MOJA (01)

1.0.1 SIFA ZA MWOMBAJI

Awe na elimu ya Kidato cha nne au cha sita aliyehitimu mafunzo ya Astashahada/Cheti (**NTA LEVEL 5**) Katika moja wapo ya fani zifuatazo: Utawala, Sheria, Elimu ya Jamii, usimamizi wa fedha, Maendeleo ya Jamii na Sayansi ya sanaa kutoka chuo cha Serikali za Mitaa Hombolo, Dodoma au chuo chochote kinachotambuliwa na serikali.

1.0.2 KAZI NA MAJUKUMU YA MTENDAJI WA KIJIJI

- i. Afisa masuuli na Mtendaji Mkuu wa Serikali ya Kijiji;
- ii. Kusimamia ulinzi na usalama wa raia na mali zao, kuwa mlinzi wa amani na msimamizi wa utawala bora katika Kijiji;

- iii. Kuratibu na kusimamia upangaji wa utekelezaji wa Mipango ya Mendeleo ya Kijiji;
- iv. Katibu wa Mikutano na Kamati zote za Halmashauri ya Kijiji;
- v. Kutafsiri na kusimamia sera, sheria na taratibu;
- vi. Kuandaa taarifa za utekelezaji wa kazi katika eneo lake na kuhamasisha wananchi katika kuandaa na kutekeleza mikakati ya kuondoa njaa, umasikini na kuongeza uzalishaji mali;
- vii. Kiongozi wa Wakuu wa Vitengo vya Kitaalam katika Kijiji;
- viii. Kusimamia, kukusanya na kuhifadhi kumbukumbu zote na nyaraka za Kijiji;
- ix. Mwenyekiti wa kikao cha wataalaamu waliopo katika Kijiji;
- x. Kupokea kusikiliza na kutatua malalamiko na migogoro ya wananchi;
- xi. Kusimamia utungaji wa sheria ndogo za Kijiji; na
- xii. Atawajibika kwa Mtendaji wa Kata.

1.0.3 NGAZI YA MSHAHARA

Kwa kuzingatia viwango vya mishahara ya Serikali ya **TGS B** kwa mwezi

MASHARTI KWA JUMLA

- i. Mwombaji awe Raia wa Tanzania ambaye ana umri si zaidi ya miaka **45** na sio pungufu ya Miaka **18**.
- ii. **Waombaji wenge ulemavu wanahamasishwa kutuma maombi na wanapaswa kuainisha kwenye mfumo wa kuombea ajira aina ya ulemavu walionao kwa ajili ya taarifa kwa Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma.**
- iii. Waombaji waambatanishe maelezo binafsi yaliyojitosheleza **Curriculum Vitae** (CV) yenye Anwani inayotumika, namba ya simu na **Anuani ya barua pepe** (E-mail address) pamoja na majina ya Wadhamini (**referees**) watatu wa kuaminika.
- iv. “Provisional/Testimonials/Statement of results” na hati za matokeo za kidato cha nne na sita (form IV na VI result slip) **HAVITAKUBALIWA**.

- v. Waombaji wote waambatanishe cheti cha kuzaliwa kilichothibitishwa na Mwanasheria/Wakili.
 - vi. Waombaji waliostaafishwa katika Utumishi wa Umma hawaruhusiwi kuomba isipokua kama wanakibali cha Katibu Mkuu Kiongozi.
 - vii. Waombaji ambao tayari ni Watumishi wa Umma na wamejipatia sifa za kuingilia katika kada tofauti na walizonazo, wapitishe barua zao za maombi ya nafasi ya kazi kwa waajiri wao na waajiri wao wajiridhishe ipasavyo.
 - viii. Waombaji kazi ambao tayari ni waajiriwa katika nafasi za kuingilia walioko katika Utumishi wa Umma wasiombe na Wanatakiwa kuzingatia maelekezo yaliyokatika waraka **Na. CAC.45/257/01/D/140** wa **tarehe 30 Novemba 2010**.
 - ix. Maombi yote yaambatane na vyeti vya taaluma vilivyothibitishwa na Mwanasheria/Wakili ambavyo ni vyeti vya Kidato cha Nne, Kidato cha Sita kwa wale waliofikia kiwango hicho na vyeti vya kuhitimu mafunzo mbali mbali kwa kuzingatia sifa za kazi husika.
 - x. Waombaji waliosoma nje ya Nchi wahakikishe vyeti vyao vimethibitishwa na Mamlaka husika (**TCU, NACTE na NECTA**)
 - xi. Uwasilishaji wa Taarifa na Sifa za kughushi, wahusika watachukuliwa hatua za kisheria
 - xii. Barua ya maombi iandikwe kwa Kiswahili au Kiingereza
 - xiii. Mwisho wa kupokea barua za maombi ni jumatano tarehe **03 JULAI, 2024**.
 - xiv. **MUHIMU:** kumbuka kuambatisha barua yako ya maombi ya kazi iliyosainiwa pamoja na vyeti vya elimu, aidha anuani ya barua hiyo ilekezwe kwa;

MKURUGENZI MTENDAJI (W)

HAL MASHAURI YA WILAYA YA NYANG'HWALE

S.L.P.352

NYANG`HWAI F

xv. Maombi yote ya kazi yatumwe kwenye mfumo wa kielekroniki wa Ajira (**Recruitment Portal**) kupitia anuani ifuatayo; <https://portal.ajira.go.tz/> (anuani hii pia inapatikana kwenye tovuti ya sekretarieti ya Ajira kwa kuingia sehemu iliyoadikwa 'Recruitment Portal').

xvi. Maombi yatakayowasilishwa nje ya utaratibu ulioainishwa katika Tangazo hili **HAYATAFIKIRIWA.**

Imetolewa na:

Husna Toni
Mkurugenzi Mtendaji (W)
NYANG`HWALE